HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 09 Septemba - Desemba 2011

# Fursa za uwekezaji bila uwezeshwaji zina tija gani kwa wananchi wa Vijijini?

Uwekezaji katika rasilimali za nchi kama vile ardhi, madini, misitu na mbuga za wanyama ni dhana inayopigiwa chapuo sana na serikali ya Tanzania kwa mtizamo kuwa, manufaa yatokanayo na uwekezaji, yatamnufaisha mwananchi mmojammoja na hatimaye taifa zima kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kodi mbalimbali. Kwa namna sera na sheria zinavyoandaliwa na hata baadhi ya jitihada kuchukuliwa, suala la fursa za uwekezaji linaonekana ni wazi kwa kila mtanzania ingawa katika hali halisi itachukua muda si haba kwa watanzania zaidi ya asilimia 80 wanaoishi vijijini kunufaika na fursa hizi kutokana na ukweli kuwa, fursa peke yake hazitoshi bila kuwepo na mipango na michakato madhubuti ya kuwawezesha wanavijiji kutumia fursa za uwekezaji katika rasilimali zilizo kwenye maeneo yao.

Mada hii inajadili pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika mipango ya uwekezaji na kuwawezesha kwa nyenzo, ujuzi na huduma muhimu za kiuwekezaji kwenye rasilimali husika. Tofauti na hivyo, mabadiliko ya kimaendeleo kwao, hata kama yatatokea yatachukua muda mrefu kuliko inavyotarajiwa.

Serikali imeingia katika gharama kubwa za kutunga

Endelea Uk.3




*Cathbert Tomitho - Afisa Programu Kitengo cha Utafiti na Usambazaji wa Taarifa-Hakiardhi akichangia hoja kwenye Kongamano la Kilimo Kwanza-Landmark Hotel June 2011*

## NUKUU

"Hoja ya kukua kwa uchumi bado ni kiini macho kwa mwananchi wa kawaida maana tunaambiwa uchumi umekua, lakini pia umaskini umeongezeka, wasio na kazi hawakupungui bali wanaongezeka; hivi huu ukuaji wa uchumi unamnufaisha nani hasa?, aina gani ya uchumi unaokua bila maisha ya watu kubadilika? Hapa ni kuwa macho na suala la uwekezaji hasa katika ardhi"

(Na.Issa Shivji)

## YALIYOMO


- Fursa za Uwekezaji... Uk.1,3,5
- Tahariri Uk.2
- Ajira za Ujira kichele Uk. 4,5
- Nafasi ya ahadi na mikataba 6 -7
- Migogoro kati ya wananchi Uk. 8,11
- Kona ya Sheria Uk. 9
- Safu ya maoni ya wasomaji Uk. 10
- Machapisho Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi
Alice Shamge

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe
Alice Shamge - Mjumbe

**Mchapishaji**
Hakiardhi

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es Salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.
Email:
**ecoprinttz@yahoo.com**

# TAHARIRI

## Uwekezaji usiwe njia ya kupora rasilimali za taifa



*Na Yefred Myenzi*

Ni takribani miongo minne sasa tangu Tanzania ilipoingia katika mfumo wa uchumi wa soko huria katikati ya mwaka 1986 na kuruhusu sera zenye mlengo wa kibepari kuwa ndio mhimili wa maendeleo ya taifa. Kabla ya kipindi hicho, Tanzania ilijaribu kujenga mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa mlengo wa kijamaa ambao sera, sheria na kanuni za maendeleo, zililenga kujenga jamii ya watu walio sawa katika kupata haki, kutumia rasilimali na kunufaika na matunda ya maendeleo kupitia uzalishaji mali.

Leo hii hali imebadilika sana. Siasa ni ya ushindani wa vyama vingi, uchumi ni wa ushindani wa soko huria, dhana ya usawa ni katika fursa na wala sio haki inayozingatia hali ya mtu, na mgawanyo wa manufaa ya maendeleo unazingatia kiwango cha hisa alichowekeza mtu katika ardhi, vipande, kampuni ya ndege au biashara ya kusafirisha vifurushi na wala siyo usawa unaotokana na maendeleo ya ujumla ya taifa.

Katika toleo hili, tumejadili kwa kina na kwa mifano hai jinsi ambavyo wawekezaji kutoka nje ya vijiji na nje ya nchi, yaani wazawa kwa wageni wamepewa fursa za kisheria na wakati mwingine kujichukulia fursa kwa uwezo wao wa kifedha na kimamlaka kuvuna mali na rasilimali za wanavijiji bila kujali haki za wenyeji hao, usawa wala uwiano katika mgawanyo wa manufaa ya uwekezaji husika. Wapo waliopewa mapori ya misitu wakavuna mbao na magogo kisha kutelekeza ardhi tupu na kutokomea kusikojulikana, na wapo pia waliogawiwa mashamba ya chakula ili wapande miti wauze hewa safi ya oksijeni kutokana na miti. Tusisahau kuwa wapo wawekezaji waliopewa vitalu vya uwindaji wakafikia hatua ya kuhamisha wanyama hai kama Twiga kwenda nchini kwao bila kuzuiwa na askari wala wenye dhamana wa nchi hii.

Hayo yote yakitokea, mwananchi wa kijijini anabaki kuwa kibarua au kwa lugha ya zamani manamba kwenye shamba aliloporwa na mwekezaji huyu mharibifu wa mazingira na anakosa muda wa kuzalisha hata chakula chake ili ajikimu. Ujira aupatao haumuwezeshi kujikimu na kumudu mahitaji mengine ya kimaisha kwa vile ni ujira kichele mno. Bila shaka uwekezaji wa namna hii, wa kukwapua mapori, kusafirisha wanyama hai, kuharibu mazingira, kubadili matumizi ya ardhi bila kujali mahitaji ya wananchi na kuwageuza wanavijiji kuwa manamba, hauwezi kulifikisha taifa katika ndoto ya kimaendeleo iliyo katika vitabu vyake kama dira 2025. Uwekezaji huu wa kiuporaji hauna budi kusitishwa ili kuirejesha nchi katika ndoto zake za awali za kujenga jamii ya watu walio sawa na huru na wanaonufaika kwa pamoja na matunda ya uhuru wao. Ni dhahiri kwamba hatujafika hapa kwa bahati mbaya, bali ni kutokana na ubovu wa mifumo ya uwajibikaji ambayo inaruhusu yasiyotakiwa kuanzia ngazi ya sera, sheria, kanuni na hata utekelezaji wa yale yaliyoandikwa vitabuni. **Ni jukumu letu sote kubadili hali hii, na kwavile haiwezi kutokea kimazingaombwe, basi anza wewe kunuia kuleta mabadiliko kisha wengine watafuata.**

# Fursa za uwekezaji bila uwezeshwaji

*Inatoka uk. 1*

sera, sheria na kuweka mikakati mingi ya muda mfupi na mrefu ikiwa ni pamoja na kuendesha mikutano na maonyesho makubwa kuhusu uwekezaji ndani na nje ya nchi. Hayo yote ni jitihada anuai katika kutangaza vivutio vya uwekezaji vilivyopo nchini ambavyo haviwezi kubezwa. Suala la kujiuliza hapa ni kwa kiasi gani promotion hizo za fursa za kiuwezekaji zimefanyika vijijini kwa wahusika na kwa namna gani wao wenyewe wameshiriki katika kuibua mawazo na mbinu wanazoona zitawasaidia kupiga hatua japo moja mbele. Tumeshuhudia ziara nyingi za viongozi nje ya nchi wakitangaza vivutio vya uwekezaji lakini juhudi kama hiyo haifanywi ndani ya nchi kikamilifu. Ndio maana ukienda vijijini utawakuta wananchi wakisubiri wawekezaji waje kuchukua madini, ardhi ya misitu, magogo, mafuta, wanyamapori na hata wadudu na wao wawe vibarua wa kuchuma hizo rasilimali.

Inawezekana uwekezaji kwa tafsiri yake ukaonyesha tija lakini kutokana na utekelezaji wa aina hii ukawa ni hasara na kilio kwa wananchi na taifa kwa jumla. Ni jambo la muhimu sana kutafakari nafasi na manufaa ya mwananchi na taifa katika uwekezaji wowote ule.

Suala jingine muhimu hapa linahusu manufaa ya uwekezaji. Je, ni sahihi kwa mfano kwa wawekezaji wakubwa katika kilimo cha nishati uoto, mazao ya chakula, maua na katika ranchi za mifugo kuwa ndio wanufaikaji pekee wa rasilimali hizo? Je haiwekezani wananchi nao kuwa wabia kwa kutumia ardhi na rasilimali hizo kama mitaji yao kwenye ubia? Bila shaka jibu ni rahisi tu kuwa endapo watawezeshwa kwa taratibu za kisheria, miundombinu, rasilimali fedha hasa kupitia mikopo nafuu na elimu ya ujasiriamali, watakuwa wabia muhimu tu jambo ambalo kwa sasa halifanyiki.

Katika maeneo mengi ya vijijini, manthalani katika wilaya za Kilwa, Kisarawe, Rufiji, Bagamoyo, Kilindi, Korogwe, Hanang na kwingineko, kunasikika vilio vya wananchi walio wengi wakinyanyasika na uwekezaji mkubwa katika maeneo yao kutokana na mfumo huo. Kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za ardhi na haki za binadamu. Wawekezaji wameharibu mifumo asilia ya maisha ya wazawa wa maeneo waliyoyatunza kwa miaka mingi kabla ya kuyakabidhi kwa wawekezaji hawa.

Mfano mzuri ni katika kijiji cha Mavuji, Wilaya ya Kilwa ambako sehemu ya wanavijiji wamekuwa ombaomba wa chakula kutokana na kugawa ardhi kubwa kwa kampuni ya Bioshape kwa ajili ya kilimo cha jatropha kama ilivyo katika vijiji 11 vya Wilaya ya Kisarawe ambavyo viligawa ardhi inayofikia hekta 9,000 kwa kampuni ya Sunbiofuel. Wawekezaji wote wawili walitoa ahadi za kuboresha maisha ya wanavijiji kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapa ajira, kujenga visima vya maji, kushirikishana teknolojia ya kilimo ili kuboresha ulimaji wao, kujenga zahanati, barabara na madaraja. Hata hivyo, ahadi zote hizi zimekuwa hewa na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kulinda maslahi ya wananchi hawa. Ndipo inapooneka dhahiri kuwa hata fursa zinazotokana na uwekezaji wenyewe zisiposimamiwa haziwezi kuwanufaisha wananchi hususan wanavijiji wanaotoa ardhi na rasilimali zao kwa wawekezaji.

Kukosa uwezeshaji kumewapora wananchi hata ile fursa ya kukabiliana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na wawekezaji. Hili liko dhahiri hasa katika uwekezaji kwenye sekta ya madini. Mfano mzuri ni katika Wilaya ya Tarime kwenye mgodi wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya African Barick Gold Tanzania limited. Eneo hili limeshuhudia vitendo visivyo vya kibinadamu vinavyohatarisha maisha ya wananchi kama vile kuachia maji yenye kemikali za sumu kutoka katika migodi hadi kwenye mto Tigite unaotumika kwa matumizi ya binadamu na wanyama

*Endelea Uk.5*




*Eneo ambalo Mwekezaji amepewa kufanya utafiti Kijiji cha Talawanda- Bagamoyo*



# Ajira za Ujira kichele katika Mashamba ya nishati uoto hazina tija kwa wenyeji

*Na Alice Shamge*

Katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na wimbi la wawekezaji wanaongia nchini kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwemo mahoteli, viwanda na kwenye mashamba makubwa ya jatropha, miwa, michikichi na mazao mengineyo. Uwekezaji huu mkubwa unatokana na sera za nchi kuruhusu sekta binafsi kuwa mhimili wa uchumi wa taifa badala ya dola ambayo imebakiwa na jukumu la kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo kwa ujumla wake. Pamoja na mambo mengine yanayoongelewa kuhusu mchango wa uwekezaji kwenye sekta hizo zote, navutwa kuzungumzia suala la ajira za wenyeji katika uwekezaji wa mashamba makubwa hususan mashamba ya nishati uoto - 'biofuel'. Yapo mengi katika hili lakini nitapenda kujikita katika mambo matatu muhimu ambayo ni **aina za ajira hizo, ujira unaotolewa na mazingira ya utendaji wa kazi** kwa watanzania wanaopata ajira hizo.

Nikianza na hili la aina za ajira, ukweli ni kwamba wawekezaji wengi wanahitaji nguvu kazi kwa ajili ya shughuli za awali za kusafisha mashamba, kuchimba mitaro na barabara, kung'oa visiki na kupalilia magugu hasa kwa maeneo ambayo utaalamu wa kutumia madawa kuua magugu haujaanza kutumika.

Tafiti zilizofanywa katika maeneo mbalimbali yakiwemo Wilaya za Kisarawe, Kilolo, Mufindi na Kilwa ambako uwekezaji wa aina hii umefanyika, zimebaini kuwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka maeneo ya wawekezaji ndio wamekuwa wakipata ajira hizo maarufu kama 'ajira za mtulinga' huku ajira za kitaalamu zikitolewa kwa watu wanaotoka mbali na maeneo hayo.

Mfano hai ni katika Wilaya ya Kisarawe ambako kampuni ya Sunbiofuel kutoka Uingereza imepewa eneo la uwekezaji lenye ukubwa wa hekta 9,000. Kampuni hii iliahidi kutoa ajira za muda mfupi na za kudumu kwa wananchi wasiopungua 5,000 wakati wa kuomba ardhi kwenye vijiji 11 ambako uwekezaji huu unafanyika. Hata hivyo, kwa miaka mitatu ambayo kampuni hii imeendesha shughuli zake tangu 2009 hadi 2011, imeweza kutumia eneo la ukubwa wa hekta 2,000 na kuajiri wafanyakazi wa muda na wa kudumu wapatao 750 ambao hata hivyo ajira zao zimekuwa hazina uhakika kutokana na mwekezaji kutaka kuuza mradi wake na kuwaachisha kazi hizo. Nilibahatika kutembelea mradi huu katika baadhi ya vijiji hasa vya Mtamba, Mhaga na Chakenge na kuwakuta vibarua ama wakisafisha mashamba au wakipalilia na kunyunyiza dawa kwenye mimea ya jatropha iliyokuwa tayari kuanza kutoa mazao.

Aina hii ya ajira za muda mfupi haina uhakika kwa kuwa ni lazima waajiriwa walipwe kwa wiki au wiki mbili ili kukwepa kuwaingiza katika mifumo ya mifuko ya hifadhi za jamii kama vile NSSF, n.k. Katika mfumo wa kibepari ambao ndio hasa wawekezaji wanaoutumia, sharti uwe na jeshi kubwa na vibarua wa aina hii maana hao ndio rahisi kuwalipa ujira mdogo na kuwafanyisha kazi kwa muda mrefu ili kupata faida zaidi. Ieleweke kwamba sehemu kubwa ya vibarua hawa mfano - Sunbiofuel, Kisarawe ndio waliokuwa wamiliki wa ardhi na mashamba yaliyochukuliwa na mwekezaji akiahidi kulipa fidia ambayo hata hivyo, kati ya shilingi milioni 840 alizoahidi kulipa, ni shilingi milioni 240 tu ambazo alimudi kuzilipa kama fidia ya eneo lote la hekta 9,000 na kuzua migogoro baina ya wanavijiji wanaotaka kujua mustakabali wao baada ya maeneo yao kuchukuliwa.

Suala la pili na muhimu pia ni kuhusu ujira unaotolewa kwa aina ya kazi zinazofanywa na vibarua. Kwa ujumla, vibarua katika mashamba makubwa yawe ya jatropha, miwa au misitu wanalipwa kiasi kidogo sana ukilinganisha na kazi wanazozifanya. Mfano mzuri ni kampuni ya New Forest inayowekeza katika mradi wa upandaji wa miti katika Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa. Wafanyakazi ambao huanza kazi saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni hulipwa kati ya shilingi 2,000 na 5,000 kwa siku kulingana na aina ya kazi. Kazi ambazo vibarua walikutwa wakizifanya ni pamoja na; kujaza udongo katika viroba vya kupandia miti, kufyeka mashamba, kuchimba mashimo ya kupanda miti, kupalilia mashamba, kung'oa visiki na kutengeneza njia za kuzuia moto.

Kipato hicho ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya wenyeji katika vijiji na kata zinazozunguka mashamba Endelea Uk.5



*Wafanyakazi wa Kampuni ya Bioshape - Kilwa wakiongea na watafiti na waandishi wa habari kuhusu kero za uwekezaji*

# Fursa za uwekezaji bila uwezeshwaji

*Inatoka uk. 3*

wa nyumbani na kusababisha athari za kiafya.

Msomi wa jamii Profesa Issa Shivji akihoji juu ya maendeleo na manufaa kwa wananchi yanayodaiwa kutokana na uwekezaji kwenye tamasha la jinsia lilifanyika mwaka 2011 katika viwanja vya Mtandao wa jinsia Tanzania vilivyoka Mabibo jijini Dar es salaam, alikaririwa akisema; "hoja ya kukua kwa uchumi bado ni kiini macho kwa mwananchi wa kawaida maana tunaambiwa uchumi umekua, lakini pia umaskini umeongezeka, wasio na kazi hawakupungui bali wanaongezeka; hivi huu ukuaji wa uchumi unamnufaisha nani hasa?, aina gani ya uchumi unaokua bila maisha ya watu kubadilika? Hapa ni kuwa macho na suala la uwekezaji hasa katika ardhi".

Bila shaka na hasa kwa mtizamo wangu, nafasi na manufaa ya uwekezaji katika kukuza uchumi wa nchi unaoambatana na kuimarika kwa maisha ya wananchi wa matabaka yote utatokana na ushirikishwaji madhubuti katika maamuzi juu ya rasilimali na wala si kwa kuwashirikisha wasomi na wanasiasa peke yao bali wananchi wote. Kwa mujibu wa katiba ya nchi ibara ya 8(1a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Lakini wananchi wamekuwa hawashirikishwi katika maamuzi mbalimbali ikiwemo suala la uwekezaji na kusaini mikataba na hivyo kuwa nje ya wigo wa manufaa ya uwekezaji.

Kwa kuhitimisha, ni lazima mikakati ya makusudi iwekwe na kutekelezwa katika kuhakikisha kuwa rasilimali zilizotunzwa na wananchi kwa miaka mingi zinakuwa na manufaa kwao. Hilo linawezekana kwa kuweka uwiano kati ya manufaa ya kibiashara na yale ya wananchi kujikimu kwenye rasilimali zao katika mifumo ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo mingine inayosimamia uwekezaji katika sekta zote. Tuanze na sheria ya uwekezaji ya 1997 tuje kwenye sheria za ardhi za 1999, sheria za wanyamapori 2009 na hatimaye sera na sheria za madini za 2010.

Taifa ni lazima lijijengee mazingira ambayo yatamuwezesha kila Mtanzania kunufaika na uwekezaji katika rasilimali za nchi ama kwa kushiriki yeye mwenyewe moja kwa moja au kupitia ubia na ikishindikana katika hayo mfumo wa kodi umwezeshe kupata manufaa zaidi kuliko ilivyo sasa. Ushirikiano wa hiari kati ya wawekezaji na wananchi kamwe hautawainua wananchi wala taifa lililojaa rasilimali kama hili lakini ambazo hazibadilishi maisha ya wananchi wake.

# Ajira za Ujira kichele katika Mashamba

*Inatoka uk. 4*

hayo makubwa utabaini kuwa hakitoshelezi kabisa mahitaji ya wafanyakazi hasa kwa sababu kubwa tatu. Kwanza baada ya kuanza kwa miradi mikubwa kama hiyo, bei ya bidhaa hasa mahitaji ya kawaida ya kila siku kama vile unga, sukari, mchele, sabuni, mafuta ya taa na ya kupikia, katika maeneo ya wenyeji hupanda mara dufu. Pili ongezeko la watu hasa watafuta ajira kutoka maeneo mengine husababisha bidhaa kuwa adimu na hivyo bei kupanda holela na Tatu, familia nyingi za kiafrika na hasa katika maeneo haya ya miradi ya mashamba makubwa ni za watu wengi hivyo kipato cha mtu mmoja huweza kugawanywa kwa wahitaji lukuki ndani ya familia yake kubwa.

Suala la mwisho na muhimu zaidi ambalo ni vema likapewa kipaumbele na mamlaka husika ni mazingira ya kazi. Maeneo mengi ya mashamba haya makubwa, yanatishiwa na masuala ya kijamii kama vile maradhi, kukosekana kwa usalama, uhasama kati ya wenyeji na wageni wanaofika kutafuta ajira, makazi duni na mengine mengi. Hii inatokana na ukweli kuwa panapokuwa na mwingiliano wa watu, ni vema serikali ikaweka huduma muhimu za kutosheleza mahitaji kama vile dispensari, huduma za vyoo, shule na nyinginezo muhimu. Hali iliyojitokeza katika eneo maarufu kama kambi ya mayai kijiji cha Mtamba Wilayani Kisarawe ilikuwa inatishia uhai na usalama wa maisha ya mwanadamu yoyote maana lilikuwa eneo linalohifadhi uhalifu wa kila aina vikiwemo wizi, upikaji pombe haramu na ukahaba.

Ili kulinda haki na maslahi ya wenyeji wanaotoa maeneo yao kwa wawekezaji , ni vema basi serikali kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa ikaweka utaratibu utakaowabana wawekezaji kuingia mikataba ya ajira na wafanyakazi inayoainisha maslahi ya mfanyakazi hata pale ambapo ajira yake itafikia ukomo.

Aidha, ni vema pia utaratibu huo huo ukatumika katika kuwabana wawekezaji kutimiza ahadi zao za kutoa ajira kwa wenyeji badala ya kuwapa wananchi matumaini makubwa ya ajira wakati wa kuchukua ardhi yao na kushindwa kutimiza ahadi hizo mara baada ya kuanza shughuli rasmi katika maeneo husika

Tumeona pia wananchi wenyeji wakishindwa kupata ajira kutokana na vigezo vya kukosa ujuzi. Kwa vile mfumo wetu wa elimu hautoi fursa ya kupata ujuzi wa moja kwa moja hasa kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari, wawekezaji wawekewe taratibu za kutoa mafunzo ya kujenga ujuzi kwa wenyeji ili hata wakikosa kuajiriwa katika mashamba yao basi waweze kujiajiri wenyewe.

Mwisho, uwekezaji mzuri ni ule ambao wenyeji wanakuwa sehemu ya maendeleo ya maeneo husika. Na hili litawekezana tu pale ambapo badala ya kunyang'anywa ardhi ili wawe vibarua kwenye ardhi yao wenyewe, watatumia ardhi hiyo kama mtaji wao na kuingia ubia na wawekezaji. Fedha ya ujira ijapokuwa nyingi haidumu kama ujira unaotokana na ubia kwenye mradi wa uwekezaji.



*Na Saad Ayoub*

# Nafasi ya ahadi na mikataba kati ya Wawekezaji na Wananchi Vijijini

Tanzania ni taifa linalotajwa kwa kujaaliwa rasilimali chekwa za kimaendeleo ambazo wachumi wenye fani wanaamini kinadharia ya kuwa Tanzania ina silaha kali za kuufukuza na kutokomeza kabisa umasikini uliowaganda watu wake miaka 50 sasa tangu uhuru wa December 9, 1961. Usawa na haki katika milki ya ardhi ni njia moja wapo muhimu katika kudumisha amani ya nchi yetu, kwa maana hiyo hata uwekezaji wetu unatakiwa kufanywa kwa umakini wa hali ya juu, ili tusije wapa ardhi watu kwa ahadi zisizotekelezeka zitakazo wapelekea Watanzania kuwa ombaomba au watumwa wasio na haki yoyote katika ardhi yao.

Uingiaji wa mikataba kati ya wananchi na wawekezaji hasa maeneo ya vijijini umekuwa ni jambo la kawaida kwa siku za karibuni. Hata hivyo, mikataba mingi imekuwa na sifa moja kubwa ya kutozingatia uwiano na usawa kati ya pande mbili zinazoingia mikataba hiyo. Na kwa bahati mbaya, upande wa wananchi ndio umekuwa ukilemewa na mzigo wa mikataba kutokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya thamani ya kitakachovunwa na mwekezaji baada ya kuingia mkataba husika na hata utaalamu wa kuandaa mikataba.

**Baadhi ya ahadi ambazo wawekezaji wamekuwa wakitoa wakati wanatafuta ardhi vijijini ni pamoja na; nafasi za ajira, kuongeza kipato kwa wananchi, maendeleo ya vijiji, kuboresha utaalam wa kilimo, ujenzi wa shule, barabara, zahanati, visima vya maji pamoja na nishati umeme.**

Baadhi ya ahadi ambazo wawekezaji wamekuwa wakitoa wakati wanatafuta ardhi vijijini ni pamoja na; nafasi za ajira, kuongeza kipato kwa wananchi, maendeleo ya vijiji, kuboresha utaalam wa kilimo, ujenzi wa shule, barabara, zahanati, visima vya maji pamoja na nishati umeme. Hata hivyo, ahadi hizi mara nyingi zimekuwa hazitekelezwi hasa kutokana na mambo mawili. Kwanza, ahadi hizi huwa si sehemu ya masharti ya uhawilishwaji wa ardhi ya vijiji ili kumilikishwa wawekezaji. Kwa maana nyingine, wawekezaji hawalazimiki kutimiza ahadi hizo kwa vile hata wasipofanya hivyo, ardhi waliyokwisha ipata hawawezi kunyang'anywa. Hivyo utekelezaji wa ahadi kama hizo kwa mfumo huu, hauna nguvu ya kisheria. Uzoefu unaonyesha kuwa, wanavijiji huweka masharti wakati wa kupitisha azimio la kutoa ardhi kwa wawekezaji wakiamini kuwa masharti hayo yatakuwa sehemu ya mkataba wa umilikishwaji ardhi unaofanywa na serikali kuu kupitia kamishina au Kituo cha uwekezaji. Hata hivyo, kwa vile muhtasari wa mkutano wa kijiji hutumika hasa kipengele kimoja tu cha kuridhia utoaji wa ardhi na wala si sehemu nyingine yoyote ya muhtasari basi masharti hayo huwa hayaangaliwi kuwa na maana yoyote. Ndio maana ipo muhtasari ya mikutano ya vijiji ambayo inaonyesha mahudhurio ya wanavijiji 52 na wengine 176 lakini ambao waliidhinisha uhawilishwaji wa ardhi ya kijiji kuwa ya jumla.



*Shamba lililopadwa miti ya misonobari kwa ajili ya hewa ukaa na Kampuni ya New Forests Wilayani Kilolo, Iringa*

Jambo la pili, hata pale ambapo wanakijiji huingia mkataba tofauti na ule wa milki ya ardhi aliyopewa mwekezaji, bado uwiano wa maslahi katika mikataba ya aina hiyo umeonekana kutozingatia haki za wananchi. Hii inatokana na ukweli kuwa, wananchi wanakosa utaalamu wa kuandika mikataba. Upo ushahidi wa mikataba iliyoingiwa kati ya wawekezaji na mwenyekiti wa kijiji kwa lugha ya kiingereza katika mazingira ambayo yanaonyesha kabisa kuwa mwenyekiti wa kijiji husika hakuwa mwelewa wa lugha iliyotumika.



*Shamba la Jatropha la Mwekezaji wa Kampuni ya Prokon Wilayani Mpanda*

Baadhi ya mifano inahusisha kampuni ya Bioshape ya Uholanzi ambayo kabla ya kupata ardhi waliyoomba mwaka 2006 ipatayo hekta 75,000 ilitoa ahadi nyingi kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa mamia, kulipa fidia nono, kutengeneza miundombinu na kuzalisha zaidi ya megawati 25 za umeme ambazo zingeweza kusaidia zaidi ya kaya 500 za vijiji vya Kilwa lakini haikuwa hivyo baada ya kupata eneo hilo. Miaka mitano baada ya kuzinduliwa kwa mradi huo mkubwa, shamba la Bioshape likazalisha kiasi kidogo mno cha mimea na kufilisika, na kusababisha ahadi za ajira na nyinginezo kwa wanavijiji kutokutimia, na kushuhudia kiasi kidogo cha ahadi za kulipwa fidia kutokana na ardhi yao na hatimaye kupelekea uhaba wa chakula na wimbi kubwa la umasikini katika jamii hiyo. Sasa huu ni mfano mmojawapo tu wa ahadi zisizo timizwa na wawekezaji punde wanapopata ardhi.

Kwa kutumia mfano huu, ni vema wananchi wakafanya mambo matatu muhimu. Kwanza, kuingia mikataba na wawekezaji bila kulazimika kuhawilisha ardhi yao ya kijiji kuwa ardhi ya jumla. Hii itawasaidia kuendelea kuwa wamiliki wa ardhi hiyo chini ya usimamizi wa serikali ya kijiji huku wakiendelea kupata manufaa yatokanayo na uwekezaji. Pili, wananchi wanapaswa pia kuwa makini wakati wa kujadiliana maslahi ya kimkataba ili kile ambacho wawekezaji wanavuna kutoka kwenye ardhi yao, kiwiane na manufaa wanayoyapata wananchi. Ni lazima wawekezaji wawe na wajibu mkubwa wa kuboresha na kusaidia shughuli za kijamii na kiuchumi (mf. ajira, kipato,ujenzi wa shule, zahanati, barabara n.k.) na makubaliano yawe yanasimamiwa na kuwe na mikataba inayofungwa kisheria kuzilazimisha kampuni kutekeleza ahadi hizi ili zisije kuziacha jamii katika mazingira mabaya. Na mwisho, wananchi wanapaswa kutofautisha kati ya ahadi wanazotoa wawekezaji nje ya mkataba wao wa kumiliki na kutumia ardhi na zile zinazotolewa kama sehemu ya mkataba wa kupewa na kumiliki ardhi husika. Hayo yote yakifanyika, ahadi na mikataba kati ya wawekezaji na wananchi vitakuwa na tija kwa pande zote mbili na nyingine zinazohusika.

# Migogoro kati ya Wananchi na Wawekezaji hadi lini?



*Na Beatha Fabian*

Ni ukweli usiopingika kuwa ardhi ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya Watanzania hasa wazalishaji wadogo kwani kutokana na ardhi wanaweza kulima, au kufuga, kwa ajili ya kujipatia kipato na chakula kwa ajili ya familia zao na wakati mwingine, kuna jamii ambazo kwa asili yao hutumia ardhi kwa matumizi mseto kama vile jamii ya Wahadzabe. Hata hivyo, kwa takribani miongo mitatu sasa, kumeibuka suala la uwekezaji wa aina mbalimbali kwenye rasilimali hizo ambao umeibua migogoro isiyoisha kati ya wananchi watumiaji, wahifadhi na walinzi wa asili wa rasilimali hizo na wawekezaji wa kuja katika maeneo hayo. Makala hii inachambua japo kwa ufupi, kiini hasa cha baadhi ya migogoro ya ardhi na rasilimali zake kuchukua muda mrefu sana kuisha licha ya jitihada za wadau mbalimbali kujaribu kuitatua kwa wakati.

Nchini Tanzania, masuala yote ya uwekezaji yanasimamiwa na kuratibiwa kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997 ambayo inatoa mwongozo na kuunda chombo maalumu kwa ajili ya shughuli za uwekezaji maarufu kama Kituo cha Uwekezaji, yaani TIC. Moja ya majukumu ya kituo cha uwekezaji ni kuhahikisha kuwa inakuwepo ardhi kwa ajili ya uwekezaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 6(C) cha Sheria hiyo. Ardhi hii inatakiwa kupatikana katika mojawapo ya makundi matatu ya ardhi ya Tanzania ambayo ni ardhi ya jumla, ardhi ya hifadhi au ardhi ya kijiji kwa kufuata taratibu za upatikanaji wa ardhi zilizowekwa na sheria za ardhi. Hata hivyo, hali ya utekelezaji wa shughuli za uwekezaji hususan upatikanaji wa ardhi isiyofungamanishwa na milki au maslahi ya mtu yoyote, umekuwa ukikinzana na madhumuni yaliyobainishwa katika sheria husika. Kwa mfano, sheria inatamka kuwa uwekezaji utafanywa katika maeneo yasiyo na maslahi ya kimakazi wala kuendeshea maisha ya kila siku ya wananchi isipokuwa kunapotokea ulazima wa kutwaa maeneo hayo kwa maslahi ya taifa. Cha kushangaza, tumeshuhudia uwekezaji ukifanywa katika ardhi inayotumiwa na wanavijiji kuendesha maisha yao au hata maeneo ya pembezoni mwa miji ambayo pia ni kitovu cha maisha endelevu kwa jamii kubwa ya wananchi wa kipato cha chini.

Matokeo yake, kumeibuka wimbi la migogoro inayohusisha wananchi na wawekezaji hasa kutokana na ukweli kuwa anapotokea mwekezaji wa namna yoyote katika maeneo hayo, wananchi hulamizika kuhama au kuhamishwa kwa nguvu ili kumpisha.

Baadhi ya migogoro ya aina hiyo na iliyodumu kwa muda mrefu ni pamoja na mgogoro kati ya jamii ya wafugaji wa vijiji 8 vya Wilaya ya Ngorongoro hasa tarafa ya Loliondo dhidi ya mwekezaji wa kampuni ya Ortello Business Corporation (OBC) ambao umedumu tangu mwaka 1992 hadi sasa (2011) bila kupata suluhu ya kudumu.

Katika mgogoro huu, wananchi wakazi wa vijiji hivyo ambavyo ni Piyaya, Arash, Maaloni, Ololosokwan, Oloipiri, Olerien-Magaiduru, Soitsambu na Losoito wanaishi katika eneo la ardhi za vijiji ambalo pia limetengwa kuwa pori tengefu la Loliondo na kumilikishwa kama kitalu cha uwindaji kwa mwekezaji huyo. Mgongano wa matumizi ya ardhi kati ya wanavijiji na mwekezaji ndio hasa umekuwa kiini cha mgogoro usiokwisha. Wakati mwekezaji anataka wafugaji waondoke ili awinde wanyama na kuendesha biashara za kitalii kwa uhuru, wananchi kwa upande wao wanataka kuona maslahi ya shughuli zozote za kitalii yanawanufaisha hata wao moja kwa moja.

Aidha, wananchi katika vijiji hivyo wamekuwa wakipinga mpango wa kuwaondoa kwa muda ili kupisha uwindaji ufanyike kisha kurejea katika maeneo hayo kwa vile kitendo hicho kinaonekana kuwa ni unyanyasaji na ukiukwaji uliokithiri wa haki zao za msingi ikiwemo ya kuishi na kupata riziki zao bila kubugudhiwa.

Suluhu pekee inayoonekana kuafikiwa na wananchi ni kuandaa mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi na kuhakikisha kuwa mgawanyo mpya wa matumizi ya ardhi na rasilimali zilizomo, unazingatia misingi ya haki na usawa kwa pande zote zinazohusika.

Eneo la pili ambalo limevuta migogoro mingi kati ya wananchi na wawekezaji ni kwenye kilimo cha mazao ya kibiashara, nishati uoto na upandaji wa misitu kwa ajili ya miradi ya kuondoa hewa ya ukaa. Matumizi ya ardhi kubwa na maji kwa ajili ya umwagiliaji vinachangia kuibua migogoro ya aina hii. Mfano hai ni mgogoro kati ya wawekezaji wa mashamba ya miwa katika bonde la Kiru mkoani Manyara Wilaya ya Babati -Mukesh Oghad na Surendra Natha Odedra dhidi ya wananchi wenyeji wa eneo hilo kama ilivyo kwa mgogoro mwingine kati ya wananchi wa vijiji vya Namwawala na Mofu Wilaya ya Kilombero dhidi ya wawekezaji wa kilimo cha miwa wanaotaka kupanua eneo la kilimo hadi ndani ya ardhi za vijiji hivyo.

Kwa upande wa nishati uoto, upo mfano hai wa wananchi wa kijiji cha Mavuji Wilayani Kilwa ambao ardhi yao inayofikia hekta 36,000 ilichukuliwa na mwekezaji wa jatropha

**Suluhu pekee inayoonekana kuafikiwa na wananchi ni kuandaa mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi na kuhakikisha kuwa mgawanyo mpya wa matumizi ya ardhi na rasilimali zilizomo, unazingatia misingi ya haki na usawa kwa pande zote zinazohusika.**

*Endelea Uk.11*

*Kona ya Sheria*

# Taratibu za uwekezaji kwenye Ardhi



Na Joseph Chiombola

Leo katika kona ya sheria, tunachambua taratibu za uwekezaji tukilenga katika kujibu hoja za wasomaji wetu wengi wa kona hii ambao walitaka kujua kwanini kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za uwekezaji katika ardhi hususan vijijini? Kwanza tunaeleza kuhusu dhana ya uwekezaji, aina na taratibu zake, kisha kudodosa baadhi ya sababu kwanini taratibu hizo hukiukwa.

### Maana ya uwekezaji

Uwekezaji, kwa mujibu wa fungu la 2 la sheria ya uwekezaji nchini unamaanisha uanzishwaji wa shughuli mpya au kuendeleza iliyopo kwa kuiongeza, kuibadilisha mfumo au kukarabati biashara iliyopo. Uwekezaji waweza kuwa ahadi ya fedha au mtaji wa kununua vyombo vya fedha au mali nyingine ili kupata faida kwa namna ya riba, kipato au kuthamini thamani chombo. Shughuli za uwekezaji hufanyika katika maeneo mbalimbali nchini na ardhi imekuwa ndio msingi mkuu wa kuwezesha uzalishaji mali katika shughuli za uwekezaji. Utaratibu mzima wa uwekezaji nchini huratibiwa na kituo cha uwekezaji nchini kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika fungu la 2 la sheria ya uwekezaji nchini ya mwaka 1997.

### Aina za wawekezaji

Sheria hiyo ya uwekezaji inatambua wawekezaji wa aina mbili ambao ni wawekezaji wa ndani na wa nje ambapo wawekezaji wa ndani hutakiwa kuwa na mtaji usiopungua dola laki moja za kimarekani (sawa na kiasi cha shilingi milioni 160) wakati wa nje wanatakiwa kuwa na mtaji usiopungua dola laki tatu za kimarekani (sawa na shilingi milini 480). Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 nayo imetoa mwongozo wa masuala mbalimbali yanayohusiana na taratibu za uwekezaji katika ardhi. Taratibu hizo zimeainishwa kama ifuatavyo:

### Taratibu za uwekezaji katika ardhi

Kwanza mwekezaji atahitaji kupeleka mpango wake wa uwekezaji katika kituo cha uwekezaji nchini ambapo kituo kitaupitia mpango huo ili kujiridhisha kama mwekezaji amekidhi vigezo vyote vya uwekezaji nchini. Mpango huo huainisha kiasi cha ardhi ambacho mwekezaji atahitaji kukitumia kwa ajili ya shughuli ya uwekezaji wake.

Pili, mara baada ya maombi ya mwekezaji kupitishwa na kituo cha uwekezaji nchini, kituo kinatakiwa kumpatia mwekezaji ardhi kutoka katika benki ya ardhi iliyopo chini ya kituo cha uwekezaji nchini. Umiliki huo wa ardhi kwa mwekezaji asiye mtanzania humilikishwa ardhi hiyo kwa kupewa hati hafifu kama ambavyo imeainishwa katika fungu la 19(2) la sheria ya ardhi maana mwekezaji harusiwi kumiliki ardhi nchini Tanzania kwa hati kamili kwa mujibu wa fungu la 20(1) la sheria ya ardhi namba 4 ya mwaka 1999 kama ilivyorejelewa na sheria namba 2 ya mwaka 2004.

### Kwanini taratibu hukiukwa?

Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za upatikanaji wa ardhi nchini Tanzania kwa ajili ya uwekezaji kutokana na ukweli kwamba benki ya ardhi iliyo chini ya kituo cha uwekezaji nchini bado haijawa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya wawekezaji hivyo kuwaruhusu wawekezaji kuzunguka nchini na kutafuta maeneo yatakayowafaa kwa uwekezaji wao wenyewe. Mara baada ya kupata maeneo hayo wawekezaji hutakiwa kufuata taratibu za kuwaomba ardhi wale wanaowakuta na kufuata taratibu maalumu ikiwemo kuwasilisha maombi katika halmashauri ya kijiji husika na maombi hayo kujadiliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Hapa ndipo makosa hutokea maana baadhi ya wawekezaji wamekuwa wakishinikiza, kushawishi na hata kujikuta wakishiriki mikutano ya vijiji hata kugonga mihuri yao wakati mikutano hiyo inapaswa kuwa huru bila mashinikizo ya mtu asiye mwanakijiji.

Maombi hayo yakisharidhiwa na mkutano mkuu wa kijiji muhutasari wa mkutano mkuu wa wanakijiji hupelekwa wilayani ambapo huangaliwa kama umekidhi vigezo vikiwemo vya ukubwa wa ardhi inayoombwa. Endapo taratibu zinakuwa zimefuatwa maombi hayo huwasilishwa kwa kamishna wa ardhi ambaye hufanya taratibu za kuhawilisha kwa kumpelekea ushauri Rais kisha mwakezaji humilikishwa ardhi na Kituo cha uwekezaji kwa kupewa hati hafifu ya milki. Utaratibu huu pia unahusisha ulipaji fidia na hakuna mwekezaji anayeruhusiwa kuanza shughuli zake kabla ya kulipa fidia kamili, ya haki na kwa wakati.


Uzoefu unaonyesha kwamba utaratibu huu huwa haufuatwi kama ulivyoainishwa katika sheria hizo hivyo kumekuwa na wawekezaji ambao wamemilikishwa ardhi kwa kupatiwa hati kamili ya miaka 99, 66, au 33 kama mtanzania mwingine yeyote anavyoweza kumiliki wakati taratibu hazikufuatwa.

Vile vile utaratibu wa kuwaruhusu wawekezaji kwenda kuomba ardhi kwa wanavijiji umekuwa ukigubikwa na vitendo vya rushwa na ukiukwaji wa haki za ardhi kwa wanavijiji. Wapo wawekezaji wamepatiwa ardhi kutokana na msukumo wa viongozi wa kisiasa ambao wamekuwa wakiambatana nao katika kuhakikisha maombi hayo yanafanikiwa.

Pia wanavijiji wengi kutokana na kuwa na uwezo mdogo kiuchumi wamekuwa wakikubali kupokea rushwa na kugawa ardhi hiyo kwa mwekezaji bila kujali matumizi yao ya sasa na baadaye katika ardhi hiyo. Pamoja na hayo yote, uelewa mdogo wa sheria za ardhi kwa wanavijiji na hata kwa wawekezaji unawafanya kushindwa kuelewa madhara ya utoaji wa ardhi hiyo kwa mwekezaji. Hii ni pamoja na kukosa uwezo wa kufanya majadiliano na mwekezaji ili kuweka uwiano katika manufaa ya kiuwekezaji kwa pande zote.

Ni vema basi viongozi na vyombo ambavyo vimepewa mamlaka ya usimimazi wa ardhi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya haki na kwa kujali maendeleo endelevu ya jamii husika. Viongozi wasiohusika na masuala ya ardhi wala uwekezaji waache kuingilia masuala ya ardhi na kuyatolea maamuzi maana vitendo vyao vina athari kubwa kwa haki za ardhi kwa wananchi wa kawaida. Serikali itekeleze jukumu lake kwa vitendo kwa kutoa elimu ya masuala ya ardhi ili kuwajengea wananchi uwezo wa kutosha wa kufanya maamuzi na kuhoji masuala yahusuyo mustakabali wa maisha yao. Ikumbukwe kuwa ardhi kwa mwananchi wa kawaida, ni uhai.

# Safu ya maoni ya wasomaji



## Migogoro baina ya Wanavijiji na wawekezaji dawa ni elimu zaidi kwa pande zote

*JOSEPH LUPA - HAKIARDHI*

Migogoro mingi inayojitokeza hapa nchini baina ya wanavijiji na wawekezaji inasababishwa na kutoheshimu mamlaka na taratibu zilizowekwa, pamoja na udanganyifu wa baadhi ya wawekezaji na kukosa elimu kwa wananchi na baadhi ya viongozi wa vijiji kuwasaliti wananchi wao.

Kama mkutano mkuu ndio wenye kuamua, ama kutoa au kukataa kugawa ardhi, iweje wawekezaji waanzie ngazi za juu kuomba ardhi badala ya kwenda kijijini moja kwa moja? Kwanini wanavijiji wanapokea barua zao? Kwanini wawekezaji wanatoa ahadi mbalimbali hata kama wanajua hawawezi kuzitimiza ili mradi waweze kupata ardhi? Ni kwa vile wananchi wanakuwa hawaelewi, basi wanawakubalia tu.

Ndiyo maana mwisho wa siku wanaposhindwa kutimiza ahadi ndio migogoro inapoanzia. Kwa kutumia mbinu ya kuandika mikataba kwa lugha ya kigeni tena kiingereza cha kisheria kwa wananchi wakawaida ambao hawajui lugha hiyo, ni wazi kwamba mwisho wa siku wananchi wanaposhtuka ndipo vurugu za kupinga huibuka. Hivyo elimu tu ndio dawa kwa pande zote.



## Migogoro ya wananchi na wawekezaji

*Bw. MOHAMED MASUDI MSENA - RUFIJI - KIJIJI KIVINJA A*

Migogoro inatokana na wananchi kushindwa kuelewa serikali inawakabidhi vipi wawekezaji ardhi ya kijiji pasipo wao kufahamu. Pia tatizo la wananchi kutofahamu thamani ya ardhi yao limekuwa ni chanzo cha wananchi kugawa ardhi kiholela. Uelewa mdogo wa sheria na thamani ya ardhi ndio tatizo kubwa kwa viongozi wa kijiji.

Kwa upande wa wawekezaji wao pia hushindwa kutimiza ahadi wanazotoa wakati wanaomba ardhi katika vijiji. Wapo viongozi wa vijiji wanaopokea hongo kutoka kwa wawekezaji hawa hali inayopelekea migogoro linapotokea tatizo kati ya wananchi na wawekezaji viongozi hawa kushindwa kusimamia haki.

Madhara ya migogoro ya wawekezaji na wananchi katika kijiji chetu cha Kivinja A ni pamoja na mapigano ya kugombea vyanzo vya maji baina ya wakulima na wafugaji kutokana na wawekezaji kuelekeza maji yote katika mshamba yao.



## Kero ya uwekezaji mji mpya KIGAMBONI

*Bi. MAHIDA SICHUDI*

Tatizo kubwa la uwekezaji katika eneo la Kigamboni ni kuhusiana na mradi wa mji mpya. Mpaka sasa tuko njia panda na tuna wasiwasi kutokana na mambo mengi serikali inafanya kwa siri. Hatujui mradi unaanzia wapi unaishia wapi, fidia ni ngapi inahusu nini ali mradi tu kero kutuweka roho juu kwenye majumba yetu yenyewe haya ya kurithi.

Sisi wala hatupingani na mradi ila tunachotaka ni UWAZI. Tujue faida na hasara za mradi mbona hatuambiwi? Suala la sisi kujua haki yetu ni wajibu wa serikali wala siyo jambo la kufanya kwa hiyari. Tunafahamu kuwa hawa wawekezaji watafaidika sana na mji wa kibiashara watakaoujenga sasa kwa nini serikali isitufikirie na sisi tunaoyaacha maeneo yetu. Je sisi hatusitahiki kufaidika na rasilimali yetu?



## Uwekezaji kwenye fukwe za bahari

*MAUA HASSANI – KIGAMBONI*

Ukiacha mji mpya kuna uwekezaji kwenye fukwe za bahari ambao umeziba njia za asili za wenyeji kupita na kusababisha maeneo ya fukwe kuzuiwa na wananchi kwa matumizi ya wazi kama zamani. Lakini kwa upande mwingine, wapo wawekezaji wa kilimo cha maua ambao huwapatia ajira vijana za kupanda, kupalilia na kuvuna maua. Angalau wanapata riziki zao ingawa shughuli za uwekezaji kwa ujumla zinaleta usumbufu mkubwa kwa maisha ya wananchi kuliko faida.



## Ajira hazitolewi kwa Wenyeji

*RAMADHANI SALUM – YALEYALE PUNA, PEMBA MNAZI*

Hapo zamani nilikuwa naelewa kuwa uwekezaji ungewasaidia watu wote, wale wa hali ya chini na wa juu. Lakini kwa mtazamo wa sasa ni wazi kuwa uwekezaji haujatupeleka popote kutokana na kuwa ajira tunazopewa hazina tija sana kwetu.

Mwekezaji akishachukua eneo hatoi tena kipaumbele kwa wananchi wa pale na ahadi zile ambazo alizitoa hapo awali hatimizi. Hata hizo ajira zenyewe zinatolewa kwa wageni tu na watu wa maeneo yale wanaachwa pasipo ajira yoyote.

Athari kubwa ni pamoja na miundombinu ya maeneo yale kuendelea kuharibika kwa kiasi kikubwa pasipo wawekezaji hao kusaidia kuiboresha. Huduma za jamii pia zinaendelea kuwa duni. Kwa kigamboni hasa maeneo ya Puna, hali ni mbaya kwa wenyeji kutokana na wawekezaji hasa wanaonunua ardhi na kuihodhi tu na wengine kidogo kujenga.

# Migogoro kati ya Wananchi na Wawekezaji hadi lini?

*Inatoka uk. 8*

lakini akaitelekeza na kushindwa kulipa hata vibarua waliokuwa wakiandaa mashamba hayo.

Ikumbukwe kuwa, mradi kama huo pia umekuwa ukitekelezwa katika Wilaya ya Kisarawe ambako mwekezaji aliyepewa hekta 8,000 katika vijiji 11 vya Wilaya ya hiyo, amesitisha ajira za wafanyakazi wake wote, huku akidaiwa kutolipa fidia kamili, ya wakati naya haki kama inavyotakiwa kisheria. Madai ya wananchi na waliokuwa wafanyakazi wa kampuni kwa pamoja yameibua mgogoro mkubwa katika Wilaya hii jirani na jiji la Dar es Salaam ambayo sasa imekuwa kimbilio la wawekezaji wa kila aina hasa wakitokea jijini au wakiwezeshwa na wenyeji wa jiji la Dar es Salaam.

Miradi ya hewa ya ukaa nayo imeibua migogoro kati ya wawekezaji na wananchi hasa katika maeneo ya vijiji vya Uchindile Wilayani Kilombero na Mapanda Wilayani Mufindi ambao ardhi yao kubwa imechukuliwa kwa kilimo cha miti kwa ajili ya miradi hii na mwekezaji kutoka nchini Norway. Masuala yanayoibua migogoro ni pamoja na ulipwaji wa fidia usiiozingatia haki pamoja na mikataba ya manufaa ya miradi hiyo ambayo inaonekana kutokuwa wazi kwa utaratibu wa ugawaji


**Ifike wakati sasa wenye dhamana wasimamie haki ili wananchi waachane na migogoro kati yao na wawekezaji na badala yake washiriki kwenye uzalishaji ili hatimaye wanufaike na rasilimali zao.**

wa ruzuku na gawio baada ya mauzo ya hewa hiyo.

Kwa upande wa sekta ya madini, ipo mifano hai ya migogoro kutoka maeneo ya Nyamongo Tarime, Buzwagi Kahama, Simanjiro (Tanzanite) Manyara, pamoja na maeneo yenye vito ambako kunachimbwa kokoto na mchanga kwa matumizi ya ujenzi. Wachimbaji wakubwa katika maeneo haya, licha ya kupewa maeneo hayo bila wananchi kushirikishwa kikamilifu, wanahusishwa na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za binadamu yakiwemo mauaji ya raia na uharibifu wa mali zao pamoja na mazingira.

Mifano hii michache kutoka kwenye baadhi ya maeneo ya uwekezaji imejaribu tu kutoa picha halisi ya kiini cha tatizo la migogoro ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji. Udhaifu ulio katika mifumo ya sheria za uwekezaji, ardhi, madini na maliasili ni chanzo kikuu cha migogoro hii kwani mara nyingi, wawekezaji wanapewa maeneo husika bila kuwashirikisha wananchi wanaoishi na kutumia rasilimali husika. Hata pale ambapo sheria zimeweka taratibu bayana za upatikanaji na matumizi ya rasilimali hizi, bado usimamizi na ufutiliaji wake umekuwa hafifu sana kiasi cha wenye nguvu kujiamulia mambo yao dhidi ya wanyonge. Aidha, kwa maeneo ambayo kiwango cha uelewa wa wananchi juu ya haki zao kwenye rasilimali hizo ni mdogo, basi wajuaji wachache wakiwemo watendaji wa serikali wametumia fursa hiyo kuwakandamiza wananchi na hivyo kuchochea migogoro ya ardhi na rasilimali zake.

Ifike wakati sasa wenye dhamana wasimamie haki ili wananchi waachane na migogoro kati yao na wawekezaji na badala yake washiriki kwenye uzalishaji ili hatimaye wanufaike na rasilimali zao. Uamuzi wa serikali kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji unaweza kuleta suluhu ya haraka zaidi kuliko njia zote za mikato zinazotumika kutuliza migogoro kila inapoibuka bila kuipa suluhu ya kudumu.



*Sehemu ya ardhi aliyopewa mwekezaji wa mradi wa hewa ya ukaa kwenye kijiji cha Kitete, Wilayani Kilombero*

# HAKIARDHI ARDHI NI UHAI



*Moja ya shamba la Mwekezaji lililotelekezwa Kijiji cha Mavuji Wilaya ya Kilwa*

**Anuani/Ofisi**
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org

## MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 2. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 3. | Haki za Wamaasai waishio Hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga |
| 4. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 5. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika |
| 6. | The Silences in the NGO Discourse - Occasional Paper No. 1 - May, *2006* | Issa G. Shivji |
| 7. | The Mute Plunder 'Bioresources & dispossession in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 8. | Public Perceptions on Bio Resources Conservation in Tanzania Occasional Paper No. 2 - Julai, *2008* | HAKIARDHI |
| 9. | Accumulation by Land dispossession and Labour Devaluation in Tanzania 2011 | HAKIARDHI |
| 10. | Maswali na Majibu yanayohusu mfumo wa milki na usimamizi wa ardhi nchini "Kitini cha Kujielimisha" 2011 | HAKIARDHI |
| 11. | Muongozo wa mafunzo juu ya sheria za ardhi na utawala katika muundo wa Serikali za mitaa 2011 | HAKIARDHI |
| 12. | Maswali na Majibu yanayohusu Migogoro ya Ardhi nchini - 2011 | HAKIARDHI |